# SHULE YA SEKONDARI LOWASSA

MKOA WA ARUSHA
Mawasiliano yote kwa:
Mkuu wa shule
Simu: 0755374354

Email;lowassasecondaryschool@gmail.com

S. L. P 03
Mto wa Mbu
Arusha
Tanzania
Afrika Mashariki

**KUMB. Na. LSS/MON/ADMN/VOL I** **22/11/2024**

**MZAZI/MLEZI WA ……………………………………………**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LOWASSA WILAYA YA MONDULI MKOA WA ARUSHA MWAKA 2025**

## 1.0.Utangulizi

Ninayo furaha kukujulisha kuwa, mwanao amechaguliwa kujiunga na **Kidato cha Kwanza** katika Shule hii **mwaka 2025**.

Shule ya Sekondari Lowassa ipo umbali wa (kilomita) **Km. 65** Kusini Magharibi mwa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana katika kituo Kikuu cha mabasi Arusha, teremka **Makuyuni mjini** au katika kibao cha Shule ya Lowassa Sekondari ambacho kiko mkono wa kushoto kama unaelekea Mto wa Mbu na Karatu kilomita mbili **(Km 2)** kutoka Makuyuni mjini.

Shule hii ni ya **Bweni** na ina wanafunzi wa Kidato cha **KWANZA** hadi cha **NNE** wavulana na wasichana pia inapokea wanafunzi viziwi na wenye ulemavu wa viungo.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza **tarehe 06/01/2025 Jumatatu**, mwanao anatakiwa kufika/kuripoti shuleni **Tarehe 05/01/2025 kabla ya saa 7:30** mchana. Mwanafunzi asiporipoti shuleni hadi ifikapo **Tarehe 31/01/2023,** mzazi/mlezi utakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria kwa kumchelewesha/kumnyima mtoto haki yake ya msingi ya kupata Elimu. Aidha endapo utampeleka mwanao shule binafsi toa taarifa mapema kwa Mkuu wa shule au katika ofisi ya Afisa Elimu Sekondari wa Wilaya ili kuepuka usumbufu wa kukamatwa.

## 2.0.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1.SARE ZA SHULE:

**Wavulana:**

(i) Suruali mbili (2) za rangi ya **Benjamin,** zenye upana wa **inchi 16 chini** na iwe na pindo juu (**turn up**). Kitambaa kimeambatishwa.

CS CamScanner

(ii) Mashati mawili (2) meupe ya tetroni mikono mifupi yasiyobana mwili.
(iii) Sweta la rangi ya **Benjamin** shingo ya **V** rangi yake iwe sawa na suruali.
(iv) Soksi rangi **Nyeusi** jozi tatu
(v) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa kwa kamba jozi mbili.
(vi) Nguo ya kushindia (shamba dress) suruali mbili (2) **rangi ya maruni** za heshima na T – Shirt ya Maruni yenye kola (form six) isiyo na maandishi.
(vii) Traki suti rangi ya **maruni** zenye mistari meupe ubavuni kwa ajili ya kuzuia baridi na mbu wakati wa usiku.
(viii) Sare za michezo ni jezi 01 rangi maruni (bukta na T- shirt yake) zisizo na maandishi yoyote pamoja na raba/njumu nyeusi.
(ix) Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi wenye bakoli ya heshima pamoja na nguo za ndani (chupi) tano, taulo, tai ya rangi ya suruali yenye mistari/strips meupe, pamoja na sabuni za kuogea na kufulia.

## Wasichana:

(i) Sketi mbili (2) za rangi ya **Benjamin** za heshima, zenye **pindo (belti) la inchi 2** kiunoni na marinda box na iwe ndefu hadi kwenye kiwiko cha miguu. Kitambaa kimeambatishwa.
(ii) Mashati mawili (2) meupe ya tetroni mikono mifupi yasiyobana mwili.
(iii) Sweta la rangi ya ya **Benjamin** shingo ya **V** rangi yake iwe sawa na sketi.
(iv) Soksi rangi **Nyeupe** ndefu **mpaka kweye goti jozi tatu.**
(v) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kufungwa kwa kamba jozi mbili vyenye kisigino kifupi.
(vi) Nguo ya kushindia (shamba dress) sketi mbili (2) **rangi maruni** za marinda ndefu hadi kwenye kiwiko cha miguu na T- shirt 2 rangi ya maruni isiyo na maandishi yenye kola (form six)
(vii) Traki suti rangi **maruni yenye mistari meupe ubavuni** kwa ajili ya kuzuia baridi na mbu wakati wa usiku.
(viii) Kwa wasichana wa kiisilamu aje na hijabu nyeupe isiyo na urembo wowote inayofunika mabega tu.
(ix) Sare za michezo ni jezi 1 rangi maruni (bukta na T- shirt yake) na raba nyeusi.
(x) Khanga moja, taulo za kike za kutosha (Ped) na nguo za ndani (chupi) 5 na tai rangi ya benjamen yenye mistari/strips nyeupe.

### 2.2. MAHITAJI YA DARASANI

(i) Daftari kubwa (counter books) kumi na mbili (12).
(ii) kalamu za kutosha, mkebe wa hesabu (kofa), rula moja ndefu (sentimita 30)
(iii) Kamusi (dictionary) moja ya tafsiri ya kiingereza kwa kiingereza kwa shule za sekondari ni lazima aje na kamusi ili ajifunze kiingereza.
(iv) Vitabu vya masomo tisa ya sekondari kidato cha kwanza, vitabu hivyo ni kwa ajili ya mwanao kujisomea.
(v) Daftari kumi (10) ndogo **page (80)** kwa ajili ya mazoezi

CamScanner

**2.3. MAHITAJI MENGINE**

(i) Sahani, Bakuli, Kikombe (vyote vya bati "*555*" aluminium) na kijiko.

(ii) Ndoo ya maji ya Lita 10 ya kuogea.

(iii) Godoro **Futi 2½** kwa **inchi 3** (TANFOAM) **Tunasisitiza godoro liwe la TANFOAM na si vinginevyo**

(iv) Shuka mbili (2) za rangi ya **Pinki** kwa **wasichana** na rangi ya **Bluu bahari** kwa **wavulana**.

(v) Mto na foronya zake za rangi inayofanana na shuka, nyavu za mbu (net) na blanketi moja (skolio).

(vi) Sanduku imara la bati (tranka)

(vii) Kila mwanafunzi ni **lazima** aje na saa ya mkononi.

(viii) Raba rangi nyeupe au nyeusi (jozi moja) na ndala (malapa) za kuogea

(ix) Begi la mgongoni la kubebea madaftari

(x) Mafuta ya kujipaka,dawa ya meno,kiwi, mswaki, kitana na vifaa vingine vya usafi binafsi

**2.4. FOMU MUHIMU ZINAZOPASWA KUWASILISHWA SIKU YA KURIPOTI SHULE.**

(a) Fomu ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelezo mengine yatakayotolewa na Shule. (***Ona Kiambatanisho F.1)***.

(b) Fomu ya taarifa ya mwanafunzi ijazwe na mzazi na mwanafunzi.( ***Ona KiambatanishoF.2),***

(c) Fomu ya Daktari ijazwe na daktari wa hospitali ya serikali (Medical Examination Form) ( ***Ona Kiambatanisho F.3***.)

## 3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(iii) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni na asubuhi (preparation)

(iv) Kuwahi katika shughuli zote za shule na nyingine utakazopewa.

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa.

(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(ix) Kutunza mali za umma.

**3.1. Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Ukajifukuzisha Shule Pindi Utakapoyatenda**

CamScanner

(i) Wizi wa aina yoyote.
(ii) Uasherati na Ushoga
(iii) Ubakaji
(iv) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi, sigara ,ugoro na kadhalika.
(v) Kupiga, kupigana na kusababisha kupigana.
(vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(vii) Kudharau Bendera ya Taifa
(viii) Kupata/kusababisha ujauzito
(ix) Kuoa au kuolewa
(x) Kutoa mimba
(xi) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu
(xii) Kukataa adhabu kwa makusudi
(xiii) Kuwa na simu au kifaa cha simu ya mkononi

**MUHIMU:**

- Mzazi au mlezi unatakiwa kushirikiana na mwanao kupitia sheria zilizotajwa hapo juu ili kumwepusha mwanao asishiriki katika makosa ambayo yatampelekea kupoteza haki yake ya msingi.
- Mzazi awe tayari kumkamilishia mwanae mahitaji muhimu ya shule ili aweze kusoma kwa raha na kumuondolea adha ya kuomba ruhusa ya kurudi nyumbani kutafuta mahitaji yake au kumsumbua mzazi mara kwa mara
- **Sare zote ziandikwe jina la Mwanafunzi kwa mashine sketi,bukta na suruali ziandikwe kwenye belt kiunoni,sweta, shati, Tsheti ziandikwe kwenye kola na shuka, blanket na godoro katikati.**
- Aidha ni muhimu kuweka alama kwa kila kitu cha mwanao ili kuepuka upotevu.

Wanajumuiya wa Lowassa Sekondari wanampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kujiunga na Shule hii, hivyo wanamkaribisha ili kuendeleza, kudumisha na kuenzi Kauli mbiu yetu inayosema **"Elimu kwa Ujuzi"** (***Education for Competence***).

***ASANTE** na **KARIBU** sana!!*

……………………………

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER
LOWASSA
SECONDARY SCHOOL

CamScanner

*F. 1*

**AHADI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MALEZI YA MWANAE**

**( ijazwe na mzazi/mlezi wa mwanafunzi na kuiwasilisha shuleni)**

Mimi.................................................................... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ........................................................ninaahidi kumhudumia mwanangu na kumpatia mahitaji yake kwa wakati na kushirikiana na shule kumlea mtoto huyu. Aidha ninaahidi kwamba nitahakikisha mwanangu atasoma na kumaliza shule na hivyo sitakubaliana na utoro wa aina yoyote.

Nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha mwanangu wa **kike** hatapata ujauzito wala sitamuoza au kupokea mahari wakati wote wa masomo yake. Endapo nitakiuka ahadi hii hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu

Saini ya Mzazi/Mlezi: .................................. Tarehe: ……………………

Mawasiliano: Namba ya Simu: 1……………………………………

2……………………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI KUHUSU KUFUATA SHERIA ZA SHULE**

**( ijazwe na mwanafunzi mwenyewe)**

Mimi ……………………………………. ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha………...2025 ninaahidi kwamba, nitafuata sheria , kanuni na taratibu za Shule na kutoshiriki kwenye migomo niwapo shuleni; nikienda kinyume na Sheria hizo nichukuliwe hatua za kinidhamu kwa mujibu wa Sheria husika niliyoivunja/kiuka.

Saini ya mwanafunzi: ……………………… Tarehe: …………………..

………………………..

**MKUU WA SHULE**

HEADMASTER LOWASSA SECONDARY SCHOOL

*F. 2*

CS CamScanner

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI**
**SHULE YA SEKONDARI LOWASSA**

**TAARIFA YA MWANAFUNZI – KIDATO CHA ……………… MWAKA ………………**

1. Shule ya Msingi aliyotoka: ……………………………………………………………..
2. Jina la mwanafunzi: ………………………………………… Jinsia: Me ……. Ke ……
3. Tarehe ya Kuzaliwa: ……………………………………………
4. Namba ya Usajili: ………………………………………..
5. Kijiji atokacho: ……………………………………………………
6. Kata atokayo: ………………………………………………………
7. Mwenyekiti wa kijiji au Serikali ya Mtaa atokako: ………………………………………
   Namba ya Simu ya mwenyekiti ………………………………………..
8. Jina la Balozi atokako: …………………………………………………………………
   Namba ya Simu: ……………………………………………………………
9. Jina la Baba/Mlezi: ……………………………………………………………
   Namba ya Simu: ………………………………………………
10. Jina la Mama/Mlezi: ……………………………………………………………
    Namba ya Simu: ………………………………………………..
11. Jina la ndugu wa karibu:
    (i) Jina la ndugu: 1 …………………………………………………………..
        Namba ya Simu: ………………………………………
    (ii) Jina la ndugu 2: ……………………………………………………………
        Namba ya Simu: ………………………………………
    (iii) Jina la ndugu 3: ……………………………………………………………
        Namba ya Simu: ………………………………………

**Ninathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi.**

**Jina: ………………………………………… Saini: ………………… Tarehe: ………………**

**Mwalimu wa Darasa: ………………………… Saini: ……………… Tarehe: ………………**

**F.3**

CamScanner

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**LOWASSA SECONDARY SCHOOL**
**<u>MEDICAL EXAMINATION FORM</u>**

To be completed by Medical Officer(government Hospital) in respect of all new students to the School.

Student's name: ………………………………………………………………

Blood count (red or white): ……………………………………………….

Stool examination: …………………………………….

Urine analysis: ………………………………………….

Syphilis: ……………………………………….

T.B. Test: ………………………………..

Eye Test: …………………………………..

Ears Test: ……………………………………..

Chest: ……………………………………………

Liver: ………………………………………………….

Abdomen: …………………………………………….
(Pregnancy test for girls)

Any other physical defect: ………………………………………………………………………….

Signature: ………………………………….

Designation: ………………………………..

Station: ……………………………………..

Date: ………………………………………..

Stamp:

…………………………
**HEADMASTER**

ADMASTER
LOWASSA
DARY SCHOOL

CS CamScanner